Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

## Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# Mwongozo wa Uundaji wa Mabaraza ya Watoto ngazi za Kijiji, Kata, Wilaya na Mkoa




Disemba, 2010

© Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2010.

Kwa mawasiliano yote kuhusu mwongozo huu:

Mwenyekiti,

Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto,

S.L.P 3448,

Dar es Salaam.

Tanzania.

Simu: +255 22 213 2526

Nukushi: +255 22 212 4852

+255 22 2133647

Barua Pepe: barazawatoto@yahoo.com

**Dibaji**

Tunatoa shukrani za pekee kwa wadau mbalimbali ambao kwa njia moja au nyingine wameshiriki katika kufanikisha kuundwa kwa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wadau hawa ni pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za dini na Watoto. Shukrani za pekee pia zinatolewa kwa kufanikisha kuandaliwa kwa Mwongozo huu.

Ni tumaini letu sisi watoto kuwa, mwongozo huu utatoa mwanga na dira kwa watoto wote na wadau mbalimbali wenye mapenzi mema na watoto katika kuhakikisha ushiriki wao wa uhakika na wa kweli katika masuala yanayogusa maendeleo yao. Hivyo basi, ni wajibu na jukumu la kila mmoja wetu, wazazi, viongozi, taasisi mbalimbali zinazofanya kazi kuendeleza maisha yetu, idara mbalimbali za kiserikali na halmashauri kuhakikisha kuwa Watoto wanapata nafasi ya kutoa maoni yao na kuchangia katika mipango na mikakati inayolenga maendeleo yao.

Ninawahamasisha na kutoa wito kwa kila mmoja wetu kusoma mwongozo huu, awe mtoto au mtu mzima, kiongozi au mwakilishi wa jamii ili kufanikisha uwakilishi makini na ushiriki wa watoto katika jamii husika. Mwongozo huu unatarajiwa kutumika na halmashauri husika, zikishirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo taasisi zisizo za kiserikali, makampuni ya kibiashara na wahisani kuweza kufanikisha uundwaji na uendeshaji wa mabaraza haya. Ninawatakia mafanikio kwa kila jambo na wazo jema linalokusudiwa na Watoto.

Wenu katika Ujenzi wa Taifa,

..................................

**Mwenyekiti,**

**Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

## 1.0 Utangulizi

### 1.1 Historia

Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina historia inayoanzia katika mkutano wa watoto kutoka sehemu mbalimbali nchini Tanzania bara na visiwani waliokutana katika mkutano wa maandalizi ya Mkutano Maalum wa Baraza la Umoja wa Mataifa kuhusu watoto uliofanyika tarehe 8-10 Mei 2002. Mkutano huo wa Umoja wa Mataifa hukutanisha maraisi kutoka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa. Katika kikao cha maandalizi kilichoitishwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto wakati huo (ambayo kwa sasa inajulikana kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto) kilichofanyika mwezi Mei mwaka 2000 cha maandalizi ya kundi la watoto waliokuwa wawakilishe watoto wa Tanzania katika mkutano huo wa Umoja wa Mataifa, waliweza kutafakari ushiriki wa watoto katika masuala yanayowahusu. Masuala hayo yalihusu pamoja na mambo mengine ushiriki wa watoto katika uandaaji na utungaji wa sera na sheria mbalimbali zinazogusa haki na ustawi wao.

Changamoto zilizojitokeza katika vikao vilivyoainishwa hapo juu ndio msingi uliosababisha kuamua kuunda chombo kitakacho hakikisha ushiriki wa watoto katika ngazi mbalimbali kutoka ngazi ya familia hadi ngazi ya Taifa. Chombo hiki kilitarajiwa kuwa cha uwakilishi na utetezi katika masuala yanayogusa ustawi wa watoto yawe ya kitaifa au kimataifa. Chombo kilichoundwa kilipewa jina la Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baraza hili liliundwa rasmi mwezi Disemba, 2002 ambapo uundwaji wake umepitia mchakato mrefu uliohusisha vikao kadhaa ambavyo hatimaye kuwezesha kuundwa kwa mfumo wa uongozi, utendaji na uteuzi wa wawakilishi katika ngazi mbalimbali za Baraza. Taratibu hizo zilizokubaliwa katika vikao hivyo rasmi zilisadia kupatikana kwa Katiba ambayo ndiyo inayoongoza utendaji wa Baraza hili.

Ili kuwezesha uendeshaji rahisi na kuweka viwango vya kiutendaji vya Baraza, katika kikao cha pili cha *Kamati Kuu* ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichofanyika tarehe 23 mpaka 25 Aprili, 2003, kilipendekeza kuwepo kwa mwongozo na utumike kwa ajili ya kuwezesha kuundwa kwa mabaraza ya mikoa na Wilaya. Katika Mkutano Mkuu wa pili wa Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanyika tarehe 20 – 22 Decemba 2003, Bagamoyo mkoa wa Pwani, wajumbe walipitisha mwongozo huo wa kwanza ili uweze kutumiwa na watoto mikoani ili kusaidia kuanzisha mabaraza katika ngazi ya mkoa na wilaya.

Kuundwa kwa Mabaraza haya kunaenda sambamba na nia ya Tanzania kukidhi haja ya mikataba ya Kimataifa na kikanda ikiwemo ya Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto na ule wa Umoja Wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto. Uundaji wa mabaraza haya katika mikoa, wilaya, kata na vijiji utasaidia kukuza uwezo wa watoto kiufahamu kuhusu masuala yanayowahusu katika maeneo husika, kujenga utamaduni wa demokrasia na kuboresha dhana ya utawala bora katika kizazi hiki kinachotarajiwa kushika hatamu. Halikadhalika, mabaraza ya Watoto yatasaidia kuhakikisha Watoto wanapata fursa ya uhakika ya kujumuika, kushiriki, kushirikishwa, kutoa maoni yao, kusikilizwa na kufanyiwa kazi kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto kifungu cha 12, na 13 na kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto kifungu cha 7, 8 na 9. Tanzania ni nchi mwanachama na imesaini na kuridhia mikataba hii.

Aidha, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008 imeanisha tamko la Sera kuhusu uanzishwaji mabaraza haya katika ngazi mbalimbali. Ni muhimu kuzingatia kuwa mabaraza haya ni sehemu ya utekelezaji wa sheria ya Mtoto namba 21 ya Mwaka 2009. Katika sheria hii, pamoja na mambo mengine, ibara ya II kifungu cha 11 cha sheria hii kinasisitiza umuhimu haki ya mtoto katika kujenga hoja, na haki ya kutoa maoni, kusikilizwa na kushiriki kikamilifu katika mambo yanayohusu ustawi wake bila kikwazo chochote. Ibara ya VIII ya Sheria hii, inaainisha wajibu na majukumu ya Serikali za Mitaa katika kulinda, kukuza na kuendeleza ustawi wa Mtoto kwenye maeneo wanayoishi. Kifungu cha 94 cha ibara hii kinaweka msisitizo wa wajibu wa Serikali za Mitaa katika kusimamia na kuhakikisha ustawi na maendeleo ya mtoto. Uundwaji na usimamizi wa uendeshaji wa Mabaraza ya Watoto katika ngazi mbalimbali za serikali ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu huu unaotolewa kisheria.

### 1.2 Maana ya Baraza la Watoto

Kwa mujibu wa kifungu cha pili cha Katiba ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 'Baraza la Watoto' linajumuisha uwakilishi wa mtu yeyote ambaye ana umri chini ya miaka kumi na minane (18) aliyechaguliwa na watoto wenyewe kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bara na Visiwani. 'Haki za mtoto' zinazinazotambulika katika katiba na mwongozo huu zinamaanisha haki na stahili za mtoto zinazotajwa kwenye Katiba ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na zinazotambuliwa na kulindwa na mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda inayohusu watoto, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria na sera mbalimbali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 1.3 Malengo ya Mwongozo huu

1.3.1 Kuweka uwiano wa uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji/Mitaa;

1.3.2 Kusaidia uanzishwaji wa mabaraza kwa kutoa mwongozo wa utaratibu wa jinsi ya kuyaanzisha;

1.3.3 Kuweka mikakati itakayohakikisha ushirikishwaji wa mtoto unaokidhi haja kulingana na Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Mtoto.

## 1.4 Madhumuni ya Mwongozo

1.4.1 Kutoa utaratibu utakaohakikisha Watoto wanajenga ushirikiano wa karibu kati na baina ya watoto, vyombo vya habari, mashirika yasiyo ya kiserikali na Serikali.

1.4.2 Kusaidia Watoto kukuza na kubadilishana uzoefu na ujuzi katika kupigania haki, wajibu na maendeleo ya mtoto.

1.4.3 Kusaidia utaratibu utakaohakikisha Watoto wanashiriki katika kutetea haki za watoto na maslahi ya watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# 2.0 MUUNDO WA BARAZA

Kanuni/taratibu za uundaji wa Baraza la Kjijji/Mtaa

## 2.1 Baraza la Watoto la Kijiji

Mabazara yote ya watoto ya Kijiji/Mtaa yatafuata mwongozo huu kwa ajili ya kuanzishwa. Mwongozo huu hauzuii mabaraza ya Kijiji/Mtaa kuwa na ziada au nyongeza katika kuunda mabaraza

2.3 Afisa Mtendaji wa Kijiji/mtaa anaombwa kuandaa watoto kutoka sehemu mbalimbali katika maeneo wanayofanyika kazi. Hapa tunapenda kusisitiza kuwa watoto watoke katika sehemu mbalimbali katika maeneo wanayofanyia kazi. Hapa tunapenda kusisitiza kuwa watoto watoke katika mazingira mbalimbali na wenye historia tofauti ili kuleta uwiano. Ni muhimu pia kushirikisha idara au vitengo vinavyohusika serikalini katika eneo unalofanyia kazi na kuhakikisha kuwa wanapata taarifa kamili ya utaratibu unavyokwenda.

2.4 Katika mkutano huu ni muhimu kwa Afisa Maendeleo ya Jamii awezeshe watoto kujadili juu ya Baraza. Watoto wajadiliane na kuelewa kuhusu katiba, na umuhimu mzima wa Baraza la Watoto katika ngazi ya Kijiji/Mtaa na uhusiano wake na Baraza la Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa

2.5 Baada ya majadiliano, watoto wafuate taratibu za uchaguzi kama ilivyoelezwa katika katiba. Sifa za wawakilishi zote zimeelezwa katika

katiba lakini zaweze kuongezewa chache kwa makubaliano ya watoto wote kulingana na mazingira halisi

2.5 Baraza la kijiji/Mtaa linapaswa kuwa na wawakilishi wasiopungua Watoto 20 na wasiozidi Watoto 40, aidha jinsia izingatiwe.

2.6 Uongozi waweza kufuata utaratibu kama ilivyoainishwa katika katiba na kama itakavyokubaliwa na watoto katika ngazi ya Kijiji/mtaa

2.7 Uchaguzi waweza pia kufanywa kwa utaratibu ambao utalingana na ulio kwenye katiba endapo tu watoto wote watakubaliana na utaratibu huo na kuufanya kuwa halali.

2.8 Baraza la Kijiji/Mtaa lina mamlaka ya kuunda kamati mbalimbali ili kurahisisha utendaji wake wa kazi

2.9 Wajumbe wa Baraza la Kijiji/Mtaa wawe na umri usiozidi miaka 18 na wawe wakazi wa eneo husika.

2.10 Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa awe ndiye Mratibu wa Baraza la Watoto ngazi ya Kijiji/Mtaa

2.11 Wajumbe wa baraza la Kijiji/Mtaa wachague wajumbe watatu miongoni mwao kuwakilisha kijiji kuunda Baraza la Kata.

## 3.0 Baraza la Watoto la Kata

Mabaraza yote ya watoto ya Kata yatafuata mwongozo huu kwa ajili ya kuanzishwa. Mwongozo huu hauzuii mabaraza ya Kata kuwa na ziada au nyongeza katika kuunda mabaraza

03.1 Maafisa Maendeleo ya Jamii na Wadau wanaombwa kuandaa watoto kutoka sehemu mbalimbali katika maeneo wanayofanyia kazi. Hapa tunapenda kusisitiza kuwa watoto watoke katika sehemu mbalimbali katika maeneo wanayofanyia kazi. Hapa tunapenda kusisitiza kuwa watoto watoke katika mazingira mbalimbali na wenye historia tofauti ili kuleta uwiano. Ni muhimu pia kushirikisha idara au vitengo vinavyohusika serikalini katika eneo unalofanyia kazi na kuhakikisha kuwa wanapata taarifa kamili ya utaratibu unavyokwenda.

03.2 Katika mkutano huu ni muhimu kwa Afisa Maendeleo ya Jamii kuwezesha watoto kujadili juu ya namna ya kuanzisha Baraza. Watoto wajadiliane na kuelewa kuhusu katiba, na umuhimu mzima wa Baraza la Watoto katika ngazi ya Kata na uhusiano wake na Baraza la Wilaya, Mkoa na Taifa

03.3 Baada ya majadiliano, watoto wafuate taratibu za uchaguzi kama ilivyoelezwa katika katiba. Sifa za wawakilishi zote zimeelezwa katika katiba lakini zinaweza kuongezwa chache kwa makubaliano ya watoto wote kulingana na mazingira halisi

03.4 Wajumbe watatu toka Baraza la Kijiji/Mtaa watawakilisha wenzao katika Baraza la Kata.

03.5 Uongozi waweza kufuata utaratibu kama ilivyoainishwa katika katiba na kama itakavyokubaliwa na watoto katika ngazi ya Kata

03.6 Uchaguzi waweza pia kufanyika kwa utaratibu ambao utalingana na ulio kwenye katiba endapo tu watoto wote watakubaliana na utaratibu huo na kuufanya kuwa halali.

03.7 Baraza la Kata lina mamlaka ya kuunda kamati mbalimbali ili kurahisisha utendaji wake wa kazi

03.8 Wajumbe wa Baraza la Kata wawe na umri usiozidi miaka 18 na wawe wakazi wa Kata husika.

03.9 Afisa Mtendaji wa Kata na Diwani wawe ni miongoni mwa wajumbe 10 wa bodi ya walezi/washauri katika Baraza la Watoto la ngazi ya Kata

03.10 Wajumbe wa baraza la Kata wachague wajumbe wawili miongoni mwao kuwakilisha Kata kuunda Baraza la Wilaya.

**0.4 Baraza la Watoto la Wilaya**

Mabaraza yote ya watoto ya Wilaya yatafuata mwongozo huu kwa ajili ya kuanzishwa kwake. Mwongozo huu hauzuii mabaraza ya Wilaya kuwa na ziada au nyongeza katika kuunda mabaraza

04.1 Maafisa Maendeleo ya Jamii wanaombwa kuandaa watoto kutoka sehemu mbalimbali katika maeneo wanayofanyia kazi. Hapa tunapenda kusisitiza kuwa watoto watoke katika mazingira mbalimbali na wenye historia tofauti ili kuleta uwiano mzuri. Ni muhimu pia kushirikisha idara au vitengo vinavyohusika serikalini katika eneo unalofanyia kazi na kuhakikisha kuwa wanapata taarifa kamili ya utaratibu unavyokwenda.

04.2 Katika mkutano huu ni muhimu kwa muwezeshaji kutoka Wilayani awezeshe watoto kujadili juu ya Baraza. Watoto wajadiliane na kuelewa kuhusu katiba, na umuhimu mzima wa Baraza la Watoto katika ngazi ya Wilaya na uhusiano wake na Baraza la Mkoa na Taifa

04.3 Baada ya majadiliano, watoto wafuate taratibu za uchaguzi kama ilivyoelezwa katika katiba. Sifa za wawakilishi zote zimeelezwa katika katiba lakini zaweze kuongezewa chache kwa makubaliano ya watoto wote kulingana na mazingira halisi

04.4 Baraza la Wilaya litaundwa na wajumbe wawili kutoka katika kila Kata za Wilaya husika

04.5 Uongozi waweza kufuata utaratibu kama ilivyoainishwa katika katiba na kama itakavyokubaliwa na watoto katika ngazi ya Wilaya

04.6 Uchaguzi waweza pia kufanyika kwa utaratibu ambao utalingana na ulio kwenye katiba endapo watoto wote watakubaliana na utaratibu huo na kuufanya kuwa halali.

04.7 Baraza la Wilaya lina mamlaka ya kuunda kamati mbalimbali ili kurahisisha utendaji wake wa kazi

04.8 Wajumbe wa Baraza la Wilaya wawe na umri usiozidi miaka 18 na wawe wakazi wa eneo husika.

04.9 Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya wawe ni miongoni mwa wajumbe 10 wa bodi ya walezi/washauri katika Baraza la Watoto la ngazi ya Wilaya

04.10 Wajumbe wa baraza la Wilaya wachague wajumbe watano miongoni mwao kuwakilisha Wilaya kuunda Baraza la Mkoa.

## 0.5 Baraza la Watoto la Mkoa

Mabazara yote ya watoto ya Mkoa yatafuata mwongozo huu kwa ajili ya kuanzishwa kwake. Mwongozo huu hauzuii mabaraza ya Mkoa kuwa na ziada au nyongeza katika kuunda mabaraza.

05.1 Baraza la Watoto la Mkoa litaundwa na wajumbe 5 waliochaguliwa kutoka kila Wilaya zilizopo katika mkoa husika

05.2 Malengo ya Mabaraza haya yanaweza kuongezeka ila ni lazima yafuate malengo ya Baraza kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha kwanza na Kifungu cha Tano cha Katiba ya Baraza la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

05.3 Mtoto yeyote bila kujali kabila, dini, jinsia wala uwezo wa akili na aina yeyote ya ulemavu ana haki ya kugombea uwakilishi katika ngazi ya Mkoa endapo tu atakuwa anatokea katika Baraza la Watoto la Wilaya

05.4 Nafasi maalum nne za wajumbe wa kuteuliwa zinaweza kutolewa na wajumbe wa Kamati Kuu ya Baraza la Mkoa kama wajumbe watakuwa wametimia 20 na hakuna wajumbe wawakilishi wa makundi maalum

05.5 Baraza la Mkoa litaundwa na wajumbe watano kutoka katika kila Wilaya zilizopo katika mkoa husika.

05.6 Mabaraza yote ya Mikoa yanapaswa kuanzishwa kwa ushirikiano wa mashirika yasiyo ya kiserikali, Idara za serikali za Maendeleo ya Jamii, CBOs, na vikundi vya vijana na Watoto vilivyopo mkoani.

05.7 Watoto watachagua wajumbe wawili (2) ambao watawakilisha Mkoa ngazi ya Taifa

05.8 Wawakilishi wa Baraza mkoa wanapaswa kujumuisha wanafunzi, watoto walio nje ya shule, watoto waishio katika vituo maalum, watoto wa makundi maalum n.k

05.9 Uongozi utafuata utaratibu kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Baraza la watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

05.10 Baraza la watoto la mkoa litachagua bodi ya walezi/washauri ambayo itakuwa na wajumbe 10 kama ilivyoainishwa kwenye katiba. Katibu Tawala wa Mkoa atakuwa ni miongoni mwa wajumbe wa bodi ya walezi/washauri.

## 0.6. Wajibu wa wadau

### 06.1 Wadau wa Maendeleo

- **Serikali**
    - Kwa kushirikiana na serikali za mitaa itaimarisha marabaza ya watoto katika ngazi ya taifa na mkoa hatimaye yaundwe katika ngazi zote.
    - Kuandaa Sera na miongozo ya uundaji wa mabaraza ya watoto

Jukumu la wadau wa maendeleo ni kutoa ushauri wa kitaalamu, vifaa na fedha kwa ajili ya uundaji na uhamasishaji wa mabaraza ya watoto.

- **Asasi na mashirika yasiyo ya kiserikali**
    - Serikali za mitaa na mashirika yasiyo ya kiserikali yatashawishi watoto kuunda na kushiriki katika mabaraza yao.

### 06.1.1 Wajibu wa Mwezeshaji

Awe ni mtu ambaye hajawahi kutuhumiwa kuhusiana na udhalilishaji na unyanyasaji wa watoto katika eneo husika, awe anafanya kazi na watoto katika uundaji au uendeshaji wa mabaraza haya ana wajibu wa:

- Kuhakikisha na kuhamasisha ushiriki sawa wa watoto wote bila kujali hali yeyote ile kwa kutumia mbinu rafiki kwa watoto.
- Kuhakikisha kila mtoto anapata uhuru wa maoni na watoto wengine wanaheshimu uhuru wa watoto wenzao
- Kuzingatia katika kuwasiliana uwezo wa mtoto kiakili, kimwili na kiutamaduni na kuhakikisha watoto wengine wanaliheshimu hilo
- Kulinda na kusheshimu usiri wa taarifa za watoto, na kuwafafanulia watoto vikomo vinavyohusiana na usiri huo hasa pale inapohusisha umuhimu wa kutoa taarifa kwa vyombo vingine

- Kutumia lugha rahisi, rafiki na yenye kueleweka na kila mtoto, inapobidi kuhakikisha kuna msaada wa kuwasiliana kwa watoto wenye mahitaji maalum
- Kuheshimu maoni na nafasi ya mtoto kidesturi, mila, dini, kisiasa na kiuchumi
- Kujifunza kutoka kwa watoto na kuwafundisha mambo yanayolingana na desturi sahihi, umri na elimu zao.

**0.6.1.2 Wajibu wa watoto katika baraza:**

- Kuheshimu maoni ya watoto wengine
- Kuheshimu watu wengine, uongozi na utawala wa kiserikali na jamii anayoishi
- Kuhakikisha watoto wenzao wanashiriki kikamilifu bila kujali hali waliyonayo
- Kulinda watoto wenzao kwa kuwapa na kutoa taarifa zinazoashiria hatari inayowakabili
- Kuheshimu usiri wa taarifa za watoto wenzao kwa kuzingatia mipaka pale usiri huo unapohatarisha maisha ya mtoto
- Kuhakikisha Mabaraza ya watoto yanafanyika kwa kushiriki na kuhamasisha watu mbalimbali katika jamii kusaidia uundwaji na uendeshaji wa mabaraza

**06.2 Uratibu**

Maana yake ni kupanga uratibu wa uchaguzi kwa kushirikiana na watoto wenyewe

**Waratibu**

- **Ngazi ya kijiji/mtaa**

  Mratibu atakuwa Afisa Mtendaji wa kijiji/mtaa

- Ngazi ya kata

  Mratibu atakuwa Afisa Mtendaji Kata/Afisa Maendeleo ya jamii

- **Ngazi ya wilaya**

  Mratibu atakuwa Afisa Maendeleo ya Jamii

- Ngazi ya mkoa

  Mratibu atakuwa ni Mshauri wa Maendeleo ya Jamii Mkoa

  Pamoja na uratibu huo wana wajibu wa

  - kutafuta rasilimali za uendeshaji uchaguzi

- Kuandika na kusambaza taarifa ili kuwezesha zoezi la uchaguzi kufanikiwa katika eneo lake
- Kufanya ufuatiliaji na tathmini.

**Wazazi/walezi**

- Kuhamasisha na kutoa ruhusa kwa watoto kushiriki katika uundaji wa mabaraza
- Kuwasaidia watoto kushiriki katika uundaji wa mabaraza

**Wajibu wa bodi ya ushauri**

- Kupokea rufaa nakuzishughulikia
- Na nyingine kama zilivyoainishwa katika katiba ya watoto kifungu na.11.5.

**06.3. Haki na Wajibu wa wajumbe wa Baraza**

- Kwa kuzingatia katiba ya watoto kifungu Na. 5.4.1,

a,b,c na d haki za wajumbe zimeainishwa, na wajibu wa kipengele 5.4.2 a,b,c yameainishwa.

- Kuheshimu maoni ya mtoto
- Kuheshimu watu wengine, uongozi na utawala wa serikali na jamii
- Kuhakikisha watoto wenzake wanashiriki kikamilifu bila kujali hali waliyo nayo
- Kulinda watoto wenzao ikiwemo kuwapa na kutoa taarifa inayoashiria hatari inayowakabili
- Kuheshimu usiri wa taarifa za watoto wenzao kwa kuzingatia mipaka pale usiri huo unapohatarisha maisha ya mtoto
- Kuhakikisha mabaraza ya watoto yanafanyika pamoja na kushiriki kuhamasisha watu mbalimbali katika jamii kusaidia uundaji na uanzishaji wa mabaraza.

**07:0 Hitimisho**

07.1 Hakikisha kuwa kuna muda wa kutosha wa maandalizi ili kuepuka kuwaharakisha watoto. Kwakuzingatia pia watoto wanazo shughuli nyingi za kufanya, epuka kuwashtukiza.

07.2 Hakikisha kuwa watoto wote wanaelewa kwa nini wanashirki na wanaelewa kuwa yale watakayoamua ni ya muhimu kwani hii ndiyo njia nzuri ya kuhakikisha kuwa uzoefu na maoni ya watoto wenyewe yanasikika katika ngazi ya taifa

07.3 Kuwa na ufahamu kuhusu lengo la Baraza la Watoto kutokana na katiba inavyofafanua na elewa ni nani anatakiwa atoe

maamuzi. Ni muhimu kujua kuwa watoto ndio wenye maamuzi katika suala hili na wewe upo kama muwezeshaji tu. (Fahamu kazi ya mwezeshaji au tafuta mwezeshaji ambaye ni mtaalamu katika Haki za Watoto)

07.4 Fanya majadiliano kuwa ya kuvutia na yasiyochosha watoto. Kuwa mbunifu na mgunduzi wa mambo. Wakati unaandaa taratibu zako jaribu kufikiria kama kijana. Washirikishe watoto mapema inavyowezekana katika maandalizi ili watoe maoni yao.

07.5 Katika mikusanyiko/mikutano, hakikisha kuwa washiriki wote wanafahamiana na kujisikia huru na kila mmoja. Pia eneo wanalokutana linawafaa watoto na linafaa kwa shughuli illiyokusudiwa. Usalama wa watoto ni jambo la muhimu sana katika mikutano.

07.6 Kama kutakuwa na watoto wanaotoka mbali, basi hakikisha kuwa wamesindikizwa na mlezi wa jinsi yake (Mtoto wa kike ni lazima asindikizwe na mlezi wa kike kandhalika wa kiume asindikizwe na mlezi wa kiume).

07.7 Kama watu wakubwa watashiriki, hakikisha kuwa wamejiandaa kufanya kazi na watoto na kuwaheshimu watoto. Ni muhimu watu wakubwa wakafahamu kuwa mkutano huu ni wa watoto na wao ndio wenye maamuzi. Wanaweza tu kusaidia pale watakapoombwa kutoa ushauri katika maamuzi.

07.8 Kumbuka wajibu wako kama mtu mkubwa. Uko pale kuwezesha majadiliano. Wawezeshe watoto kutambua wajibu wako kwani hii itawarahisisshia watoto wenyewe pamoja na wote wanaoshiriki au makundi ambayo yanapata ugumu wa kutoa maoni yao. Jihusishe na hakikisha kuwa maoni yote yanayotolewa yanaheshimiwa

07.9 Tumia njia mbalimbali za uwezeshaji hasa unapofanyakazi na makundi ya watoto wanaotoka maeneo mbalimbali ya mkoa au wilaya (uzoefu walionao na mazingira waliyotoka yanayotofautiana) ili mtoto aweze kupata kitu ambacho anakifahamu na kukielewa

07.10 Jali jinsia na tamaduni katika kundi

07.11 Washirikishe watoto na vijana katika kufanya tathmini ya kazi waliyofanya

07.12 Waulize wanachofikiri kuhusu hayo majadiliano, jambo gani wamelipenda, lipi hawajalipenda? Lipi lilikuwa changamoto

kwao?  Na wanapendekeza nini? Ili kuboresha shughuli kama hii wakati mwingine.